



Hapo kale Kobe hakuwa na magamba. Mwili wake ulikuwa wazi.



Aliteseka sana nyakati za jua,
mvua na baridi.



Alitamani kujenga nyumba yake. Alikusanya miti ya kujengea.


Kobe alikuwa akitembea polepole sana.
Hakuweza kukusanya miti ya kutosha
kujenga nyumba.





Kobe aliwaza afanye nini.

Baada ya kuwaza kwa muda mrefu, Kobe aliamua afunge safari ili akatafute nyumba.



Siku moja Kobe akiwa safarini , aliona pango. Aliingia kwenye pango lile.

Kumbe pango lile lilikuwa ni la Sungurana wanawe. Kobe aliondoka, akaendelea na safari yake.




Kobe alipanda juu ya mti. Huko alifukuzwa na makinda ya ndege yaliyokuwa kwenye kiota.

Kobe aliendelea kuteseka. Jua lilikuwa kali sana.



Siku moja akiwa safarini, Kobe alikutana na Ngo'mbe akiwa bandani na wanawe.

Kobe alimweleza ng'ombe taabu anazopata. Ng'ombe alisikitika, ila hakuweza kumsaidia.



Kobe alipoondoka kwa Ngo'mbe alipita chini ya mti. Mara maji kutoka mtini yalimdondokea.

Kobe alifurahia yale maji baada ya juakali la siku ile. Alisimama mwili wote ukalowa.

Alipotembea kidogo aliona kipande cha
mti kimenasa juu ya mwili wake.
Kipande kile kilishika vizuri.



Kobe aliokota vipande vingine na
kuviweka chini, kisha akalala chali
juu yake.





Hata alipotembea juani,
vipande vile havikutoka.

Kobe aliingia kwenye maji kuoga.
Bado vipande vile vilinasa mwilini.
Kobe alishangaa.





Kobe alijisugua chini kwenye mchanga. Magamba yale ya miti na majani yalika vizuri na kuufunika mwili wake.

Kobe alifurahi sana, sasa amepata
magamba ya kujikinga na jua,
mvua na baridi kali.
Hadi leo Kobe ana magamba.

